## Sheria Inasemaje?

Hakimu anaweza tu kutoa amri ya “kukataza unyemeleaji” ikiwa utathibitisha kuwa Mshtakiwa “alikunyemelea” AU alikunyanyasa kingono. **Itakuwa ni juu ya hakimu kuamua ikiwa ushahidi unaouelezea unakidhi matakwa kisheria.**

**Ili kuthibitisha “unyemeleaji”** lazima uthibitishe kuwa Mshtakiwa alifanya mambo haya **YOTE MANNE**:

1. Mshtakiwa aidha **alikunyatia**, au **“alikutishia”**, au **alijificha** mahali fulani akipanga kukushambulia; **NA**
2. Mshtakiwa **hakuwa na sababu halali** ya kufanya hivi; **NA**
3. Mshtakiwa **amefanya hivyo zaidi ya mara moja** kwa kipindi fulani; **NA**
4. Alichokifanya Mshtakiwa kilikuwa **hatari** kiasi cha kumfanya mtu wa kawaida kuhofia usalama wake AU kumsababishia mtu wa kawaida mfadhaiko mkubwa kihisia.

**“Kukutishia”** kunamaanisha kitu ambacho kingemfanya mtu wa kawaida kudhania kwamba Mshtakiwa angekunyanyasa kingono, kukuumiza kimwili, au kukuteka nyara. Maneno ya kidhalimu au matusi au unyanyasaji **HAYATOSHI** kuthibitisha tabia ya vitisho. Kwa mfano, hakimu kwa kawaida hawezi kutoa amri kwa sababu tu mtu anakutusi au anaandika mambo machafu kukuhusu kwenye Facebook.

**Ili kuthibitisha “unyanyasaji wa kingono,”** lazima uthibitishe kuwa Mshtakiwa alifanya jambo lililoelezwa katika sheria za uhalifu kama tendo la ngono isiyo halali. Chini ya sheria hii, baadhi ya mambo unayoweza kudhania kuwa ni unyanyasaji wa kingono (kama vile kugusa kifua cha mwanamke bila ridhaa yake) hayakujumuishwa.

## Wakati gani, Nini, Wapi

### Amri ya Kukataza Unyemeleaji

- **Haihusishi** wanafamilia, watu ambao umeishi nao, na watu ambao umekuwa na uhusiano nao kimapenzi
- Inapaswa kuwasilishwa katika Idara ya Kiraia
- Lazima iwasilishwe wakati wa saa za kazi za mahakama

### Amri ya Msaada kutokana na Unyanyasaji

- Inahusisha wanafamilia, watu ambao umeishi nao, na watu ambao umekuwa na uhusiano nao kimapenzi
- Lazima iwasilishwe katika Kitengo cha Familia
- Inaweza kuwasilishwa baada ya saa za kazi za mahakama

**Mahakama ya Vermont Mtandaoni**
http://www.vermontjudiciary.org



# Kuomba **Amri ya “Kukataza Unyemeleaji”** katika Idara ya Kiraia

**Ikiwa** unazingatia kuomba **amri ya “kukataza unyemeleaji”**, tafadhali soma brosha hii yote kabla ya kuwasilisha ombi lako. Itakusaidia kuelewa namna sheria inavyofanya kazi. Neno “Mlalamikaji” linamaanisha mtu anayeomba amri. Mtu unayetaka amri itolewe dhidi yake ni “Mshitakiwa”.

**Brosha hii inatoa maelezo ya jumla. Unaweza kutaka kushauriana na mwanasheria.**

# Jinsi Mchakato Unavyofanya Kazi

Ili kuomba amri ya "kukataza unyemeleaji" itabidi ujaze baadhi ya fomu. Mojawapo inaitwa "malalamiko" na nyingine inaitwa "hati ya kiapo." Hati ya kiapo ni pale unapoeleza kilichotokea ambacho kinakufanya uhisi unahitaji amri ya mahakama. Unapaswa kuapa kwamba unasema ukweli unapoisaini. Baada ya kujaza fomu hizi, hakimu atazisoma. Jaji ataamua ikiwa ushahidi wako unakidhi mahitaji ya amri ya dharura ya muda.

**Iwapo hakimu HATATOA amri ya dharura:**

1. Bado unaweza kuomba kuwa na usikilizaji ili uweze kutoa ushahidi mahakamani kujaribu kuthibitisha madai yako. Ukiomba usikilizaji, mahakama itatuma malalamiko yako, hati yako ya kiapo, na notisi ya kikao cha usikilizaji kwa polisi ili waweze kuwasilisha nakala kwa Mshtakiwa. Hii inaitwa "kuwasilisha kisheria" kwa Mshtakiwa.
2. Ukiamua kutoomba usikilizaji, malalamiko na hati yako ya kiapo huwekwa kwa siri na nakala haitumwi kwa Mshtakiwa.

**Ikiwa hakimu ATATOA amri ya dharura:**

1. Itakuwa amri ya muda tu. Usikilizaji wa kesi utapangwa kwa tarehe ya baadaye ili wewe na Mshtakiwa muweze kutoa ushahidi mahakamani na kueleza mikasa yenu.
2. Mahakama itatuma nakala ya malalamiko yako, hati yako ya kiapo, na amri ya muda kwa polisi. Kisha polisi watamkabidhi Mshtakiwa hati hizi. Hii inaitwa "kuwasilisha kisheria" kwa Mshtakiwa.
3. **HADI POLISI WATAKAPOWASILISHA NYARAKA, AMRI YA MUDA BADO HAITATUMIKA.**

# Kwenye Kikao cha Usikilizaji

Usikilizaji hautategemea tu mambo uliyoandika kwenye hati yako ya kiapo. Utalazimika kutoa ushahidi. Unaweza pia kuleta watu wengine kutoa ushahidi kuhusu kile kilichotokea. Iwapo Mshtakiwa atafika kwenye kikao cha usikilizaji, yeye pia atapata fursa ya kutoa ushahidi na anaweza kuleta mashahidi. Vikao vya usikilizaji viko wazi kwa umma. Kisha hakimu ataamua ikiwa ushahidi unakidhi mahitaji ya amri.

**Ikiwa hakimu ataamua kuwa hakuna ushahidi wa kutosha ili kutoa amri,** amri ya muda itaisha na kesi itatupiliwa mbali.

**Ikiwa hakimu atatoa amri**, itatumika kwa kipindi kifupi cha muda. Wewe na Mshtakiwa mtapata nakala ya amri mara tu baada ya usikilizaji ikiwa Mshtakiwa atakuwepo. Ikiwa Mshtakiwa hatakuwepo, polisi watalazimika kuwasilisha nakala kwa Mshtakiwa kabla ya amri hiyo kutekelezwa.

# Ikiwa Hakimu Hatatoa Amri ya "Kukataza Unyemeleaji"

Unaweza kuhisi kukata tamaa ikiwa hakimu hatatoa amri. Lakini kumbuka kuwa ni juu ya hakimu kuamua ikiwa kilichotokea kinakidhi mahitaji ya amri. Kumbuka kwamba sheria ya unyemeleaji inakusudia kuwalinda watu dhidi ya kuumizwa kimwili, kunyanyaswa kingono, au kutekwa nyara. Sheria ya unyemeleaji haizuii watu kukukosea heshima, kukutukana, kukufokea, kukukosoa au kukunyanyasa.

# Maelezo Mengine Muhimu

- Unawajibu wa kutoa maelezo kwa mahakama kuhusu Mshtakiwa, ikiwa ni pamoja na tarehe yake ya kuzaliwa ikiwa unaijua.
- Wasiliana na mahakama ili kujua mahali ambapo Idara za Familia na Kiraia zinapatikana katika kaunti yako au nenda kwenye http://www.vermontjudiciary.org.
- Taarifa yoyote ya ushahidi utakayoandika itahitaji kuthibitishwa, kwa hivyo unapaswa kuleta uthibitisho wa utambulisho unapoenda mahakamani kuwasilisha kesi.